

Tamasha la sarakasi kufanyika Jumamosi NA MWANDISHI WETU

KITUO cha Babawatoto kupyitia mradi wa Fit for Life kitafanya tamasha la maonyesho ya sarakasi ambalo limepangwa kufanyika keshokutwa jijini Dar es Salaam.

Mratibu wa mradi huo, Habiba Issa amesema tamasha hilo litafanyika Nafasi Arts Space na litakuwa na lengo la kuonyesha kazi mbalimbali na stadi walizopata vijana katika mradi huo ambao unafadhiliwa na Umoja wa Ulaya Parapanda na Ufafabrik ya Ujerumani.

"Tamasha halikuwa na kiingilio na tutaanza na warsha mbalimbali kuanzia saa tano asubuhi na baadaye saa tisa litaanza tamasha ambapo pia kutakuwa na vikundi vingine kama vile Kigamboni Community Centre, Safi group na Shada acrobatic group kutoka Bagamoyo," alisema Habiba.